NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

1 Januari 2022

Kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa

Marafiki Wapendwa sana,

Katika kipindi cha miaka ishirini na tano kilichoishia Ridván 2021, jitihada za taasisi za mafunzo kuwasaidia marafiki kukuza uwezo wao kwa ajili ya huduma zilikuwa ndiyo kiini kwa maendeleo. Mwanzoni mwa mfuatano wa Mipango ya mwisho ya kiulimwengu, tulipotoa mwito wa kutolewa kwa umakinifu wa kiutaratibu wa kubuni mbinu kwa ajili ya kufunza idadi kubwa ya waumini, taasisi zilikabiliwa na kazi ya kuandaa nyenzo zao wenyewe au kuchagua kutoka zile zilizokuwepo. Kwa jumla, taasisi ziliona ni changamoto kuandaa nyenzo mpya; hata hivyo, wale waliotumia kozi zilizoandaliwa na Taasisi ya Ruhi waliweza kupiga hatua za haraka. Kwa hiyo, kama ilivyoelezwa katika ujumbe wetu wa 28 Desemba 2005 kwenu, tuliamua kwamba vitabu vya Taasisi ya Ruhi, ambavyo vilikuwa vimethibitisha ufaaji wake, vingeunda mfululizo mkuu wa kozi za taasisi kila mahali angalau kwa kipindi kilichobakia cha mfuatano huo wa Mipango. Matumizi mapana ya kozi hizi, kadhalika na ya masomo na matini kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto na vijana chipukizi, yaliharakisha maendeleo ya mchakato wa taasisi kote ulimwenguni. Sasa, kwa kuwa ulimwengu wa Kibahá'í umeanza mfuatano mpya wa Mipango, tumezingatia tena suala la nyenzo za taasisi za mafunzo na tunapenda kuwasilisha mahitimisho yetu.

Maarifa na umaizi, sifa za kiroho na mitazamo, na ujuzi na uwezo kwa ajili ya huduma vinavyoshughulikiwa katika kozi za Taasisi ya Ruhi hubakia kuwa msingi kwa jitihada za jumuiya za Kibahá'í. Kwa hiyo, nyenzo hizi zitaendelea kuwa sura muhimu zinazojitokeza za jitihada za kielimu za taasisi zote za mafunzo wakati wa mfuatano huu mpya wa Mipango ya kiulimwengu. Tunatambua kwamba katika kipindi cha Mpango wa Miaka Tisa, Taasisi ya Ruhi itahitaji kukamilisha maandalizi yote ya nyenzo ilizochagua kuzitumia katika madarasa ya watoto, vikundi vya vijna chipukizi na vikundi vya mafunzo, na kupitia upya matoleo yote yaliyochapishwa kadiri ihitajikavyo kwa kuzingatia tajiriba. Hata hivyo, mbali na kile ambacho tayari kimefafanuliwa, haitarajiwi kuandaa nyenzo mpya za kutumika kiulimwengu.

Katika ujumbe wetu wa 30 Desemba 2021 kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara, tulionesha jinsi gani tulivyokuwa tumefurahishwa kuona hazina kubwa ya maarifa na umaizi ambavyo marafiki, wakijitahidi kufanyakazi katika mazingira anuwai ya kijamii na kiutamaduni, wakikuza vipengele vya mchakato wa ujenzi wa jumuiya. Marafiki pia wanongezeka kuwa hodari katika kubainisha mahitaji yanayohusiana na ukuaji unaoibuka kwa namna ya kawaida kutokana na jitihada kwenye ngazi za chini kabisa. Maendeleo haya yana athari kwa ajili ya mifumo ya kuandaa na kuboresha nyenzo za kielimu. Hivyo, tumehitimisha kwamba sasa lingekuwa jambo la heri

kuweka umakinifu zaidi kuelekeza uwezo kwenye kuandaa nyenzo za kielimu, hususan kuhusiana na nyenzo jazilizi na kozi tanzu.

Tulipozungumzia suala la nyenzo za elimu ya watoto na vijana chipukizi katika ujumbe wetu wa 12 Desemba 2011 kwenu, tulionesha kwamba, mbali na nyenzo ambazo ni za msingi kwa kila mojawapo ya program hizi, walimu na wahuishaji, kwa ushauriano na mratibu wa taasisi kwenye ngazi ya klasta, mara kwa mara wangeamua ikiwa vipengele zaidi vingehitajika kuongezwa ama la ili kuimarisha mchakato wa kielimu. Maendeleo ya kuvutia katika maeneo mengi ya ulimwengu yanayohusiana na kutoa elimu ya kiroho kwa idadi kubwa ya watoto na vijana chipukizi kwa hakika yamehusisha uwezo ukuao wa walimu na wahuishaji, kwa hekima kuongeza ujifunzaji wa masomo na matini yenye vipengele vinavyofaa kutegemeana na mazingira yao mahsusi. Maarufu zaidi katika hili ni vipengele vinavyohusiana na shughuli ya kisanii na miradi ya huduma. Hata hivyo, pale inapoonekana kuna haja ya kujaliza ujifunzaji wa mada fulani maalum kote nchini au katika kanda, baadhi ya taasisi zenyewe zimeandaa au kutafuta nyenzo za ziada na zimepanga kuzisambaza kwa mapana zaidi. Zana hizi za kujaliza, kwa sehemu kubwa, zimekuwa ni zana rahisi, kama vile nyimbo au hadithi. Tajiriba kama hiyo hiyo inakunjuka kuhusiana na mlolongo mkuu wa kozi, ingawa nyenzo za ziada ambazo baadhi ya taasisi zimezitambulisha kuhusiana na hili, ambazo hujumuisha makusanyo kutoka maandiko ya Kibahá'í juu ya mada maalum na uchunguzi kifani wa tajiriba husika, huelekea kuwa na asili ya utata zaidi.

Kushamiri kwa mchakato wenye msisimko wa elimu ya kiroho katika idadi iongezekayo ya klasta kutazihitaji taasisi zenye uwezo uliokuzwa vyema kusimamia uanzishwaji unaofaa wa zana jazilizi. Katika hili, taasisi lazima zijihusishe zaidi na uimarishaji wa mchakato wa kielimu na sambamba na kudumisha uadilifu wake. Hivyo zitahitaji kuzingatia hadhari mbalimbali tulizozionesha katika ujumbe wetu wa 12 Desemba 2011. Bila shaka, lazima pia zichunge dhidi ya kuwatwisha marafiki zana anuwai za nyongeza ambazo, kwa wingi wake, zingeweza, kwa kughafilika kuwatoa kwenye uwasilishaji wenye ufanisi wa nyenzo za kimsingi.

Kuhusiana na kozi tanzu, jinsi zinavyotakiwa kuibuka lazima kueleweke katika muktadha wa nguvu zilizopo katika nchi na kanda ambako mchakato wa ujenzi wa jumuiya unasonga mbele kwa nguvu. Kadiri marafiki wengi zaidi wanavyojitoa wenyewe kuendeleza shughuli mbalimbali ambazo kwazo huibuliwa na kozi za taasisi, maeneo tofauti tofauti ya ujifunzaji yahusianayo na kila moja ya shughuli hizi pole pole hupata umbo katika maisha ya watu. Baadhi ya maeneo haya ya ujifunzaji, kama yale yanayohusiana na ibada ya pamoja, kujiongezea elimu na ufundishaji, husaidiwa na Kamati za Ufundishaji za Maeneo, ambapo mengine yanayohusiana na elimu ya kiroho ya watoto, vijana chipukizi, vijana na watu wazima hulelewa na taasisi za mafunzo. Maeneo ya ziada ya ujifunzaji yanayosaidiwa na mawakala wengine nayo hujitokeza kadiri watu zaidi na zaidi wanavyojifunza kozi za juu zaidi za mlolongo wa taasisi. Wakati jitihada katika kila moja ya maeneo haya zinavyodumishwa kwa idadi iongezekayo ya marafiki, umaizi mpya unazalishwa ambao ni tofauti kwa namna kwamba unaibuka kutokana na jitihada zenye mpangilio zinazofanyika katika mazingira maalum ya kijamii na kiutamaduni. Kuna uelewa uongezekao wa ni dhana, mbinu, uwezo na mitazamo ipi ambavyo ni vya muhimu kuendeleza suala la mchakato

wa ujenzi wa jumuiya. Haya huwa ni mambo ya kuzungumziwa katika mikusanyiko ya mara moja moja inayofanywa ili kushauriana na kutafakari juu ya tajiriba zinazopatikana. Kando na jitihada ambazo watu binafsi au asasi pamoja na mawakala wanaweza kufanya ili kuitikia kwenye mahitaji haya, taasisi inaweza kuamua kuendeleza matumizi ya nyenzo jazilizi kama ilivyoelezwa hapo juu. Baada ya muda, yale mafunzo yanayopatikana huchukuliwa na asasi na mawakala wa Imani katika nyaraka mbalimbali, simulizi za matukio na chunguzi kifani ambazo, kwa ujumla wao, huunda kumbukumbu ya tajiriba inayokunjuka. Wakati kiwango cha kutosha cha hazina ya maarifa kinapopatikana, kinafanya iwezekane kuyapangilia zaidi kwa kuanzisha kozi tanzu.

Hapo nyuma tuliufananisha mlolongo mkuu na shina la mti ambalo hushikilia kozi zingine zinazochipuka kutokana nalo, kila tawi likishughulikia baadhi ya maeneo maalum ya kiutendaji. Maandalizi ya kozi tanzu kama hizo lazima yatokee baada ya muda kupitia ruwaza inayoonesha utendaji na tafakari na ambayo kwayo fikra na shughuli za ugani huenda bega kwa bega. Kuna mahitaji kadhaa kwa taasisi za mafunzo ambazo huchukua jukumu hili. Watahitaji waweze kuelewa kwa kina maudhui ya mlolongo mkuu wa taasisi na kanuni za ufundishaji zihusikazo, kuchambua kwa uwazi tajiriba zinazoibuka katika ngazi ya chini kabisa kadiri shughuli zinavyosonga mbele, kushirikiana na timu za marafiki waliojitoa kwa ajili ya maendeleo ya mambo maalum ya mchakato wa ujenzi wa jumuiya, kutenda kazi katika mtindo wa ujifunzaji na kuwachukua katika kazi zao watu binafsi wenye uwezo uhitajikao kwa ajili ya kuandaa nyenzo. Mara kila kitu kikiwa sawa, kozi tanzu ingeweza kuwasaidia marafiki kuendeleza shughuli inayohusiana na shughuli ili kuimarisha zaidi uwezo wao, na ingeweza kuchangia kuongeza mchakato unaohusika wa ujifunzaji katika maisha ya watu. Kozi hii pia hutumika kama ghala ya kuhifadhia maarifa na kama njia kwa ajili ya utangazaji wake.

Uandaaji wa nyenzo za aina hii ni zoezi tata, na bila shaka siyo lengo ambalo kila taasisi ya mafunzo huandaa kozi tanzu zake. Taasisi za mafunzo, kwa ushauriano na Baraza la Kiroho la Kitaifa pamoja na Washauri, wataamua ni wakati gani wa kuandaa au kuchukua nyenzo za ziada za kielimu kama hizo. Taasisi nyingi zitachagua tu kozi tanzu zinazofaa kwa mahitaji yao kutokana na zile zilizoandaliwa na taasisi zingine zenye ufanisi uliothibitika. Mbali na kozi tanzu, inatazamiwa kwamba hapo baadaye taasisi zitaandaa au kuchukua aina zingine za kozi, ambazo kwa namna fulani zinaweza kujumuishwa katika mlolongo mkuu au kutolewa kipekee pekee. Kwa kawaida, hili litahitaji upataji wa uwezo mkubwa zaidi kwa taasisi. Hata hivyo, bila kujali matokeo ya mbali zaidi ya jitihada zao, taasisi hazitarajiwi kushughulikia mahitaji yote ya kielimu ya jumuiya ya Kibahá'í. Ndani ya jamii anuwai, ukuaji mkubwa utasababisha kujitokeza kwa jitihada mpya za kielimu kushughulikia mahitaji mengine ya lazima.

Tuna imani kwamba, kadiri marafiki wanavyopambana katika maeneo yote kuachilia nguvu ya Imani ya ujenzi wa jamii, miaka ya usoni itashuhudia upanuzi wa kutambulika zaidi wa uwezo wa taasisi za mafunzo kutoa elimu ya kiroho kwa idadi kubwa na kuzalisha, kutumia na kueneza maarifa. Kama sehemu ya mamlaka yake kusimamia mchakato wa uzalishaji wa rasilimali watu, tumekiomba Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa kufuatilia kwa ukaribu ukuzaji wa uwezo kwa ajili ya kuandaa nyenzo za

kielimu. Kitaanzisha mifumo kwa ajili ya kuzisaidia taasisi na kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yale mafunzo yanayopatikna yanaenezwa ifaavyo.

Tutamsihi Uzuri Uliobarikiwa katika Makaburi Matakatifu ili utendaji wa taasisi za mafunzo, mawakala hawa muhimu wa Imani, ziweze kuendelea kupokea baraka na mathibitisho Yake yasiyoshindwa.

Nakala:

Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa Bodi
za Washauri
Washauri
Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Kibahá'í